



## BODI YA BIMA YA AMANA

### KATIKA SHAURI LA NJOMBE COMMUNITY BANK LTD (CHINI YA UFILISI) NA KATIKA SHAURI LA SHERIA YA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA, 2006 (THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS ACT, 2006)

#### TAARIFA KWA UMMA

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba **NJOMBE COMMUNITY BANK LTD** imewekwa chini ya ufilisi na Benki Kuu ya Tanzania kuanzia tarehe 4 Januari, 2018. Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 41 (a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, 2006 (The Banking and Financial Institutions Act, 2006) Benki Kuu ya Tanzania imeiteua Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board –DIB) taasisi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 37 (1) cha Sheria tajwa kuwa Mfilisi wa Benki hiyo.

Kufuatia uteuzi huo, Mfilisi wa **NJOMBE COMMUNITY BANK LTD**, Bodi ya Bima ya Amana (DIB), inatoa taarifa kwa wadai na wadaiwa wote wa benki hiyo kama ifuatavyo;

- (a) Wadaiwa wote wa **NJOMBE COMMUNITY BANK LTD** na mtu yoyote anayeshikilia mali ya Benki hiyo ikiwa ni pamoja na kumbukumbu au nyaraka na vifaa vyovyote vya ofisi anataarifiwa kwamba alipe madeni hayo, arudishe kumbukumbu/nyaraka na mali za benki hiyo kwa Mfilisi (DIB) kupitia anuani iliyotajwa hapo chini kabla ya siku ya Jumanne tarehe 17 Aprili, 2018. Wale watakaokaidi taarifa hii watachukuliwa kwamba wanashikilia mali hizo kinyume cha sheria kuanzia siku ya Jumanne tarehe 17 Aprili, 2018.
- (b) Vile vile, wadai wote ambao sio wenye amana (Depositors) wa **NJOMBE COMMUNITY BANK LTD** (chini ya ufilisi) wanataarifiwa kuleta madai yao yakiwa na uthibitisho kamili kwa Mfilisi kwa kutumia anuani iliyotolewa hapo chini kabla ya siku ya Jumanne tarehe 17 Aprili, 2018.

**Mkurugenzi**  
**Bodi ya Bima ya Amana**  
**Jengo la Makao Makuu ya Benki Kuu ya Tanzania**  
**2 Mtaa wa Mirambo**  
**Ghorofa ya 7, Mnara wa Kaskazini**  
**11884 DAR ES SALAAM**

Email: [DIB-INFO@bot.go.tz](mailto:DIB-INFO@bot.go.tz)  
TEL: +255 22 223 5390  
Fax: +255 22 223 4200

**IMETOLEWA TAREHE 17 MACHI, 2018**